

HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

Simu Na. 0732 988324/ 0732

988305

Fax Na. 0732 988258

Email: ded@urambodc.go.tz



S.L.P 170,
URAMBO.

Unapojibu tafadhali taja:

03/01/2018

Kumb. Na. UDC/W.I /254/27

TANGAZO LA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Urambo imepokea kibali **Kumb. Na. FA.170/365/01/83** cha tarehe **20/12/2017** kutoka kwa **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.** Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo anawatan Wananchi wenye sifa kuomba Nafasi za kazi zilizotangazwa kama ifuatavyo:-

Dereva Daraja la II Nafasi Mbili (2)

Sifa:

- Elimu ya kidato cha nne au sita.
- Awe na leseni daraja 'E' au 'C' ya uendeshaji pamoja na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitatu bila kusababisha ajali.
- Awe amehudhuria mafunzo ya uendeshaji wa magari (Basic Driving Course) yanayo tolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo chochote kinacho tambulika Serikalini.
- Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

Kazi na Majukumu

- Kuendesha magari ya Abiria na malori
- Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote, kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo.
- Kufanya matengenezo madogo madogo katika gari.
- Kutunza na kuandika daftari la safari "Log – Book" kwa safari zote.

Mshahara: TGS B

Maelezo ya Jumla

1. Waombaji wote katika barua zao waambatanishe na maelezo binafsi (CV)
2. Picha 2 za "Passpot Size" ya hivi karibuni
3. Nyaraka za Vyeti zilizothibitishwa na Mamlaka za Kisheria
4. Maombi yote yaandikwe kwa mkono.
5. Ni muhimu kuweka namba ya simu kwa ajili ya mawasiliano
6. Waombaji wote wawe na umri usiozi miaka **40** na wawe Raia wa Tanzania.
7. Tarehe ya kuanza kupokea maombi ni **05/01/2018** na tarehe **ya mwisho ni 18/01/2018, saa 9.30 Alasiri**

Maombi yote yatumwe kwa:-

**Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya,
S. L. P. 170,
URAMBO.**

Makaing'o
Margaret J. Nakainga
**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
HALMASHAURI YA WILAYA
URAMBO**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
URAMBO.**